
The Guardian

Page 3.



f hands

# Govt working on strategies to improve welfare of pack donkeys - TALIRI director

**By Polycarp Machira, Dodoma**

THE Tanzania Livestock Research Institute (Taliri) is conducting a study on donkeys in effort to improve welfare of the pack animal in the country and advice the government accordingly.

Globally, donkeys are facing a population crisis because of the huge demand for their skins, bones and meat in China, where they are used to make health foods and traditional medicine.

Donkey meat is also a popular food, but a huge drop in the number of Chinese donkeys and the fact they are slow to reproduce, has forced suppliers to look elsewhere.

Tanzania like other African countries has been badly hit because the animals are such an important part of life for transport and farming - particularly in poorer communities.

Dr Jonas Kilima, director, technology transfer and researcher at TALIRI told this paper that there is need to establish several factors affecting development of donkey in the country, noting that there is very little information about the animal.

He said his institution is working to get to know among others gestation period of the animals, the reproduction cycle in general and what best can be done to improve their welfare.

"Unlike other animals such as goats, sheep and cows, little is known about donkey, one of the domestic animals that is commonly used for transport and other duties mainly in the rural areas" he said.

According Dr Kizima, donkeys in the country have come under serious threat since establishment of donkey abattoirs in Dodoma and Shinyanga few years ago. Both facilities were started by Chinese.

He pointed out that one of the most important problems in promoting donkeys is the lack of knowledge about their socio-economic status, husbandry and health needs

While the Dodoma based abattoir is closed down, the Shinyanga one is operating at full capacity and its management has asked the government to allow them process as many donkeys as possible. It currently operates under slaughter permit of 30 donkeys per day.

Dr Kizima said during a visit to districts of Iringa,Chemba, Arusha district council, Longido and Dodoma, several farmers complained of theft of donkeys by people who reportedly transport them to the nearest abattoirs.

According the researcher, there is need to establish the best way to promote the working animals to ensure the multiplication lest they face extinction.

Dr Stanford Ndibalema, a director in the Department of Veterinary Services under the Ministry of Livestock and Fisheries noted that the government allowed slaughter of donkeys in the country because a lot of donkeys were being smuggled to Kenya

The government also believed it was losing out on potential revenues from donkeys stolen in Tanzania and slaughtered in Kenyan abattoirs for export to China.

"We found ourselves in a situation where we had no slaughter houses operating, and yet more donkeys were being stolen from Tanzania and smuggled to Kenya. There were buyers in Tanzania who were encouraging and incentivising donkey theft and smuggling into Kenya," Ndibalema said.

"With the ever-increasing number of stolen donkeys trafficked into Kenya, we decided to let the abattoirs re-open in February 2018. The idea was to let them operate while government worked out ways of regulating the industry to ensure it does not drive our donkeys to extinction."

He acknowledged that there is serious decrease of donkeys in the country, thus the need to see how to increase the number of animals.

es

Malilo
washed
s family
all his
vesting
ods.
orities
flood
flour,
h was
while
dallah
lour.

HABARI LEO UK 7.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa mwaka 2020, Bungeni jijini Dodoma juzi. (Picha na Mroki Mroki).

Scanned with CamScanner




UHURU UK 18

# Tani 20 minofu ya samaki zasafirishwa tena Mwanza

**Mwanza**
**NA BALTAZAR MASHAKA**

SIKU chache baada ya kuzinduliwa kwa safari za kimataifa kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwanza,shehena ya pili ya minofu ya samaki tani 20 imesafirishwa tena kwa ndege ya Shirika la Rwadair A330-300 yenye usajili 9xR-WP kwenda Brusels nchini Ubelgiji.

Ndege hiyo ilirejea nchini ikitokea Uholanzi na kuondoka tena na tani 20 za minaofu ya samaki ambapo gharama ya mzigo na usafirishaji umegharimu kiasi cha USD 80200 ambapo shehena hiyo ya minofu ya samaki imesindikwa na kuzalishwa kwenye viwanda viwili vya Tanzania Fish Processors Ltd (tani 16) na Nile Perch Fisheries Ltd (tani nne) ambazo zimegharimu Dola za Marekani (USD) 80200.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, akizungumza baada ya kushuhudia awamu y pili ya ubebwaji wa mzigo huo, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi jengo hilo la mizigo ambapo ndege yoyote duniani inaweza kutua katika eneo hilo.

Alisema tija ya uwekezaji huo inaanza kuonekana kwa rasilimali kutumika ipasavyo, sambamba na wenye viwanda vya samaki kuanza kuona thamani ya kusafirisha bidhaa zao nje kwa kutumia uwanja huo badala ya mizigo yao kukosa ndege na kulazimika kufuata huduma hiyo nchi jirani ya Kenya.

"Haya ni maono ya Rais Dk. Magufuli na ni maelekezo yake ya muda mfupi ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa haraka. Pia, biashara hii imeanza kufufuka na mahitaji yanazidi kuwa makubwa, hivyo wakazi wa Mwanza wachangamkie fursa hii kikamilifu,"alisema Mongela.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli ( MSCL) Eric Hamissi, alisema Tanzania kwa utajiri ilionao inaweza kufanya mambo makubwa kwa kusafirisha minofu ya samaki, lakini baadaye watasafirisha nyama ya ng›ombe na mbuzi na kupongeza mapinduzi hayo makubwa yaliyofanywa na serikali ya awamu ya tano.

Naye Meneja wa Kiwanda cha Nile Perch Fisheries Ltd, Ruesh Mohan, alisema kusafirisha mzigo kutokea Mwanza kumewapunguzia gharama za usafirishaji na kuiomba serikali kuangalia namna ya kupata usafiri huo wa ndege kwa wiki mara mbili na kwamba licha ya soko la samaki kushuka sababu ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID -19) bado viwanda vyao vina uwezo wa kuzalisha na kusafirisha tani 100 hadi 150 kwa wiki kutoka Mwanza kwenda Ulaya.

Kwa upande wake, Meneja Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Tanzania Fish Processors Ltd, Godfrey Samwel, aliwataka wavuvi kuendelea kufanya kazi za uvuvi kwa bidii na kufuata taratibu zilizowekwa na serikali kwa kuwa usafiri wa uhakika wa kusafirisha samaki kwenda Ulaya upo na soko la uhakika linaptikana.

Alisema uzalishaji utakapokuwa mkubwa usafirishaji wa bidhaa hiyo utaongezeka kwa sababu kutakuwa na malighafi za kutosha ambpo aliiomba serikali kuangalia namna ya kuwa na ndege ya ndani itakayosafirisha mzigo kwenda nchi mbalimbali za Ulaya ili kukuza uchumi wa nchi.

«Tulianza na tani nane leo tunasafirisha tani 16 za minofu ya samaki, mzigo pamoja na gharama za usafirishaji ni dola 64200, hivyo imani yetu ni kuendelea kusafirisha mzigo mkubwa zaidi kwani awali tulipata taabu kusafirisha mzigo kwa njia ya barabara kwa kutumia malori kwenda Nairobi wakati mwingine gari likiharibika njiani mzigo unaharibika na kutofika kwa muda, «alisema Samwel.

Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, Pascal Kalumbete, alisema uwekezaji wa miundombinu ya kisasa uliofanywa na serikali unawezesha ndege za ukubwa na aina yoyote kutua na kuruka kwenye uwanja huo na kuongeza kuwa jengo la mizigo lina uwezo wa kuhifadhi mizigo inayoharibika haraka (mazao mabichi) na mazao makavu na kuzitaka sekta binafsi (wawekezaji wazawa) kuchangamkia fursa hiyo na kutengeneza soko la kimataifa.



**MKAZI wa Nyakabungo, Mary Johnson, akichagua samaki aina ya sangara kwenye Soko Kuu la Jiji la Mwanza, lililojengwa kwa muda katika Kata ya Mbugani wilayani Nyamagana. (Picha na Baltazar Mashaka).**

Scanned with CamScanner

na Watoto, Dkt Godwin Mollel; Katibu Tawala (RAS) Mkoa wa Pwani, Dkt Delphine Magere; Balozi wa Tanzania Nchini Algeria, Jacob Kingu; Balozi wa Tanzania Nchini Msumbiji, Balozi Phaustine Kasike; Balozi wa Tanzania Nchini Kenya, Balozi John Simbachawene pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia General John Mbungo. (Picha na Ikulu)

MAJIRA UK 3

# *Asimulia alivyoibiwa ng'ombe, kukatwa mapanga*

**Na Dismas Lyassa, Kibaha**

MKAZI wa Mtaa wa Lumumba, Kata ya Pangani iliyopo Halmashauri ya Kibaha mkoani Pwani, Rafael Damiani Chilongozi ameelezea mkasa aliokabiliana nao Machi Mosi, mwaka huu baada ya kuvamiliwa na watu wasiojulikana kisha kumuibia ng'ombe wake na kukatwa mapanga.

"Katika maisha yangu sikuwahi kufikiria kwamba kuna siku naweza kufikwa na tukio la aina hii, kuibiwa ng'ombe na kukatwa mapanga, najiona kama mkosi, lakini naamini Mungu amenisimamia, kwani sasa naendelea vizuri na hata mifugo yangu nimeweza kupambana mwenyewe hadi kufanikiwa kuipata," alisema.

Daniamini aliyasema hayo jana katika mahojiano na mwandishi wa habari hizi katika Mtaa wa Lumumba, Kata ya Pangani Halmashauri ya Kibaha, mkoani Pwani ambaye Machi mosi mwaka huu alivamiwa na kukatwa mapanga kisha mifugo yake kuibwa na watu usiku akiwa amelala kwenye nyumba yake.

Alisema, siku hiyo usiku akiwa amelala, watu walimvamia na kuanza kumkatakata mapanga huku wengine wakianza kuwaswagwa ng'ombe wake na kuondoka nao.

"Watu hao walianza kwa kuwaswaga ng'ombe na kuondoka nao. Nikiwa nimelala, nilihisi kama nje hakuko kawaida, ikanibidi nifungue mlango kuangalia nini kinaendelea nje, kwani ng'ombe walikuwa wanapiga kelele zisizo za kawaida, ndipo nikabaini kuna wizi unaendelea. Ikabidi kuwafuatilia watu wale waliokuwa na ng'ombe, ndipo walipoanza kunikata kwa upanga,"alisema.

Akifafanua zaidi alisema ilivyokuwa ni kwamba alipoanza kuwafuatilia wezi hao, alimulikwa na tochi usoni, kisha ndipo wakaanza kumkata kwa upanga hadi akapoteza fahamu. Ni kutokana na makelele aliyopiga ndipo baadae sana majirani walimchukua na kumpeleka Polisi kisha Hospitali ya Tumbi ambako alipatiwa matibabu na sasa ameruhusiwa akiendelea na matibabu.

Kwa upande wake kaka wa Damian, Deodatus Chilongozi ambaye ndiye mmiliki wa mifugo hiyo alisema, wakati tukio hilo linatokea yeye hakuwepo. Lakini anamshukuru Mungu kwa kumsaidia kupatikana ng'ombe wake. "Mimi nimekuwa naishi eneo hili kwa zaidi ya miaka 20, sijawahi kufikwa na mkasa kama huu wa kuvamiwa na kukatwa mapanga. Ilivyo ni kwamba mimi nimekuwa mwajiriwa wa Mitamba toka 1997, hata baada ya mkataba kumalizika, nikawa nimebaki hapa naishi kama mwangalizi wa eneo lao. Eneo hili ninaloishi majirani wapo mbali.

"Natamani kama ingewezekana ningepata silaha au namna nyingine yoyote ya kupata ulinzi ili niendelee kuwa salama, kwani nilipo na majirani ni mbali. Lakini pia siwezi kujisogeza na majirani kwa sababu mifugo yangu inaweza kula mazao yao na hivyo kiingia kwenye mikwaruzo. Ombi langu kubwa ni kwa Serikali kuangalia kuniruhusu kumiliki silaha yoyote hata kama ni gobole ili niweze kujilinda kwani kitendo hiki kimeniogopesha sana," alisema Chilongozi.

zi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Malaika Kids wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 8

# Wataalamu wa uvuvi kupata ajira kimataifa

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WATAALAMU wa vyombo vya uvuvi nchini wataanza kuajiriwa kitaifa na kimataifa, baada ya Bunge kuridhia mkataba wa kimataifa wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995.

Akisoma mkataba huo bungeni jijini hapa jana, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema kuridhiwa kwa mkataba huo kutaleta manufaa tisa kwa taifa.

Dk. Kalemani alisema kwanza utatoa fursa za ajira za ndani na za kimataifa kwa wataalamu wa vyombo vya uvuvi.

Alisema pia kutahakikisha kuwapo kwa ukaguzi wa waangalizi wenye weledi ambao kuwapo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

"Kutaimarisha vyuo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika kimataifa, kuwapo kwa viwango bora vya ufundishaji wa wanafunzi katika vyuo vya uvuvi nchini," alisema Waziri Kalemani.

Alisema kuidhinishwa kwa mkataba huo kutaimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali.

"Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1994, kazi ya uvuvi ilionekana kuwa ni kati ya kazi hatari duniani kwa kusababisha wastani wa wavuvi 24,000 kupoteza maisha kila mwaka. Idadi hii ni zaidi ya mara 10 ya vifo vinavyotokea katika meli za biashara," alisema Waziri Kalemani.

Alisema mkataba huo pia utawezesha kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari pamoja na kuimarisha kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

Alisema manufaa ya kupitishwa kwa azimio hilo ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kutoa mafunzo na vyeti vinavyotambulika kimataifa katika uvuvi wa vyombo vya bahari kuu.

Waziri Kalemani alisema baadhi ya madhara yanayoweza kutokea iwapo mkataba huo hautaridhiwa ni pamoja na Watanzania kutoajirika katika nafasi za kimataifa eneo la uvuvi wa bahari kuu, kinyume na wale wanaofanya kazi katika meli za biashara.

Alisema pia Tanzania itakosa nguvu za ukaguzi na uangalizi wenye weledi kwa meli za kimataifa zinazofanya kazi katika bahari kuu kwa ajili ya kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Alisema kutasababisha kukosekana kwa usimamizi wa ulinzi, usalama na uchafuzi wa mazingira ya bahari, Tanzania kutoonekana kuwa eneo salama la kuvua samaki kwa kutofikia viwango vya kimataifa.

Alisema Tanzania itakosa mapato kutokana na kukosekana kwa ajira za Watanzania katika soko la kimataifa.

Akisoma ushauri wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hawa Mchafu, alisema ni muhimu kwa serikali kuzingatia mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi na kuiwasilisha bungeni ili kuridhiwa mapema na kuanza kunufaika badala ya kusubiri athari zitokee.

Alisema ni muhimu serikali iharakishe kuandaa sera ya bahari kwa kuwa ni muhimu hasa kama nchi inataka kuwekeza na kunufaika na uchumi unaotokana na bahari.

Vilevile alishauri Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), kuimarishwa na kuboreshwa kwa kuhakikisha linakuwa na vitendea kazi bora na vyenye kukidhi viwango vya Taifa na kimataifa kwenye kufanya ukaguzi.

Scanned with CamScanner

sanamu ya Bikira Maria na vitu mbalimbali vilivyoibwa katika makanisa ya T.A.G na Romani Katoliki mkoani humo jana.

MTANZANIA UK 3

# *Wabunge wataka chombo* kusimamia sekta ya uvuvi

Na RAMADHAN HASSAN - DODOMA

BAADHI ya wabunge wameiomba Serikali kuunda chombo maalumu cha kusimamia sekta ya uvuvi ili iweze kuinufaisha nchi.

Wakichangia mjadala wa azimio la mkataba wa kimataifa wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995 bungeni jana, waliiomba Serikali kuunda chombo maalumu cha kusimamia sekta ya uvuvi ili iweze kuinufaisha nchi.

Mbunge wa Masasi, Dk. Rashid Chuwachuwa (CCM) alisema ni muhimu Serikali ikaweka chombo maalumu cha kusimamia sekta ya uvuvi ili iweze kunufaika na rasilimali zilizopo katika eneo hilo.

"Naona ipo sababu Serikali kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kununua meli kama zile katika maziwa makuu ili kuendelea kupata kipato kikubwa.

"Ninakubaliana kwa dhati kabisa na nia ya Serikali kuleta azimio hili, naomba turidhie wavuvi waweze kutambulika katika sura ya kimataifa," alisema Dk. Chuwachuwa.

Mbunge wa Viti Maalumu, Hawa Mchafu (CCM), alisema walichelewa kupitisha azimio hilo kwani lina mambo mazuri kwa wavuvi.

"Utajiri ni mkubwa katika lugha ya Kiswahili, unatakiwa kuingia katika lugha ya Kiswahili unapokuwa na umuhimu wa azimio hili, itasaidia vyombo vya uvuvi, vitakuwa katika mikono salama," alisema Hawa.

Mbunge wa Mafia, Mbaraka Dau (CCM) alisema kwa kukubaliwa itifaki hiyo, sasa mabaharia wataweza kukubalika kimataifa.

"Wataweza kwenda kwenye zile meli kwenye bahari kuu, meli zinazokuja kuvua mpaka 100, ushauri wangu kaeni pamoja mawaziri msaidiane kutengeneza sheria nzuri," alisema Dau.

## MKATABA WENYEWE

Akisoma mkataba huo bungeni jijini hapa jana kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani alisema kuridhiwa kwa mkataba huo kutaleta manufaa tisa kwa taifa.

Dk. Kalemani alisema kwanza utatoa fursa za ajira za ndani na za kimataifa kwa wataalamu wa vyombo vya uvuvi.

Alisema pia kutahakikisha kuwapo kwa ukaguzi wa waangalizi wenye weledi ambao kuwapo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

"Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1994, kazi ya uvuvi ilionekana kuwa ni kati ya kazi hatari duniani kwa kusababisha wastani wa wavuvi 24,000 kupoteza maisha kila mwaka. Idadi hii ni zaidi ya mara 10 ya vifo vinavyotokea katika meli za biashara," alisema Dk. Kalemani.

Alisema mkataba huo pia utawezesha kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari pamoja na kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

Dk. Kalemani alisema manufaa ya kupitishwa kwa azimio hilo ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kutoa mafunzo na vyeti vinavyotambulika kimataifa katika uvuvi wa vyombo vya bahari kuu.

Alisema baadhi ya madhara yanayoweza kutokea iwapo mkataba huu hautaridhiwa, ni pamoja na Watanzania kutoajirika katika nafasi za kimataifa katika eneo la uvuvi wa bahari kuu, kinyume na wale wanaofanya kazi katika meli za biashara.

Akisoma ushauri wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hawa Mchafu alisema ni muhimu kwa Serikali kuzingatia mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi na kuiwasilisha bungeni ili kuridhiwa mapema na kuanza kunufaika badala ya kusubiri athari zitokee.

Alisema ni muhimu Serikali iharakishe kuandaa sera ya bahari kwani ni muhimu sana, hasa kama nchi inataka kuwekeza na kunufaika na uchumi unaotokana na bahari.

Vilevile alishauri shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuimarishwa na kuboreshwa kwa kuhakikisha linakuwa na vitendea kazi bora na vyenye kukidhi viwango vya taifa na kimataifa kwenye kufanya kaguzi.

Akisoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano, Susan Kiwanga, alisema mkataba huo una maudhui mazuri kwa kuwa utawafanya wananchi ambao ni wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi, kuwa na viwango vya kimataifa.

Alisema kwa kufanya hivyo kutakuwa na ushindani katika soko la ajira la kimataifa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina akichangia mjadala huo, alisema mtu yeyote ambaye atavunja sheria za nchi atakamatwa bila ya kuangalia yeye ni nani.

iliyobeba imetua k wa Kim (KIA) iki Kam taarifa waliopan kwa ba ndege 'b zimejaa. Akiz wa hab Kamwel imetua anga la huu. "N imetua Kimatai ni mwa kwa usa za kimat

Mnan mafut pamo maga Mafut kupiti Many Tangu ya Ta Hata Kaska ratibu ya Ta kumn Hivyo mikoa Mtu cha milio EWU wote

Scanned with CamScanner